

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI

Kikao Cha Tisa – Tarehe 8 Februari, 2008

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (*Mhe. Samuel J. Sitta*) Alisoma Dua

SPIKA: Tukae tafadhali. Waheshimiwa Wabunge, jana usiku, Mheshimiwa Rais, aliniita na kunifahamisha rasmi kwamba, amekubali kujiuzulu kwa Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, kama Waziri Mkuu. Baada ya hapo, akanitaarifu kwamba, kwa mujibu wa Katiba, amelivunja Baraza la Mawaziri. Ninaomba nirejee kwenye Katiba ili kuweka kumbukumbu katika hali ilio sahihi. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, Mawaziri na Naibu Mawaziri, wanaendelea na nyadhifa zao isipokuwa yaktokea mazingira yafuatayo:-

Ibara ya 57(2) inaendelea kuanzia (a) na mpaka (g), ninaomba kunukuu: “Kiti cha Waziri au Naibu Waziri, kitakuwa wazi litokeapo lolote kati ya mambo yafuatayo: Endapo mwenye madaraka atajiuzulu au kufariki dunia; ikiwa mwenye madaraka hayo atakoma kuwa Mbunge kwa sababu yoyote isiyohusika na kuvunjwa kwa Bunge; ikiwa Rais atafuta uteuzi na kumwondo kazini mwenye madaraka hayo; au iwapo atachaguliwa kuwa Spika.”

Sasa kinachohusika hapa ni 57(2)(e) inavyosema; “Iwapo Waziri Mkuu atajiuzulu.” Kwa hiyo, Waziri au Naibu Waziri, anakoma kuwa Waziri au Naibu Waziri, iwapo Waziri Mkuu atajiuzulu au Kiti chake kikiwa wazi kwa sababu nyingine yoyote. Sasa baada ya kuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, amemwandikia Rais kwamba anajiuzulu na jana jioni Rais, kukubali na kwa mujibu huu, ninadhani kwa kutumia kifungu hiki hiki cha Katiba, ibara hii hii, kulivunja Baraza la Mawaziri; kwa hiyo ni dhahiri ndani ya Bunge hili sasa hatuna Serikali. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu Serikali imebaki na watu wawili tu; Rais na Makamu wa Rais, ambao hawamo ndani ya Bunge; sasa ibara ya 63(2) ya Katiba inatamka kazi zetu kama Bunge; na kazi hizo kimsingi ni kuishauri na kuisimamia Serikali; kusimamia Serikali ni pamoja na kuwauliza maswali Mawaziri, sasa hawapo! (*Kicheko/Makofi*)

Kushauri ni pamoja na kama kuendelea kujadili haya mapendekezo ya Kamati Teule, ili tukishashauri yale yatakayokubalika, wawepo wa kuyatekeleza, hawapo! Kwa msingi huo, ninatangaza kulahirisha Bunge, nipate nafasi ya kushauriana na taasisi mbalimbali. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, ninasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni. (*Kicheko*)

Nyakati hizi sio za kawaida hata kidogo. (*Kicheko*)

(*Saa 3.05 asubuhi Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

TAARIFA YA SPIKA

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, ninapenda niwaeleze hatua zitakazofuata kutokana na shughuli tuliyu nayo mbele yetu. Hatua ya kwanza ni Spika kulijulisha Bunge, kuhusu kuitwa na Rais; niliitwa saa 10.50 Ikulu Ndogo hapa Dodoma.

Hatua ya pili, Spika kufungua bahasha mbele ya Wabunge, kusoma barua hiyo kutoka kwa Rais, inayotamka jina la uteuzi wa Waziri Mkuu, uliofanywa na Rais ili jina lipitishwe na Bunge. (*Makofi*)

Hatua ya tatu, nitamwomba Mwanasheria Mkuu wa Serikali, atoe maelezo ya utangulizi na baadaye kulisoma Azimio la Kumthibitisha Waziri Mkuu Mteule na atamalizia kama kawaida, kwa kuomba kutoa hoja. Ninadhani ataungwa mkono.

Hatua ya nne, Wabunge kuunga mkono kwa kusimama, kwa sababu hiyo nayo ni hoja, kwa hiyo, tutasimama wachache, ninatumaini tutawaona tutajadili kidogo itakuwa imeungwa mkono.

Hatua ya tano ni Spika kutoa nafasi kwa Waziri Mkuu Mteule ili aseme machache na inafanana kama kuomba kura tu.

Hatua ya sita ni kura za siri kupigwa. Tumekwishaandaa *ballot paper*, *Hansard* mpaka sasa jina hawalijui mpaka nitakapolitamka, lakini kwa sababu ni wepesi wataleta.

Hatua ya saba, kutangaza matokeo ya kura.

Hatua ya nane, nitamwomba Waziri Mkuu Mteule, aseme machache na aje kushikana mkono na Mheshimiwa Spika na baada ya hapo basi nitatoa matangazo mengine.

Kwa hiyo, sasa ninaingia hatua ya pili ambayo ni kuifungua bahasha iliyotoka Ikulu. (*Makofi*)

Ninaisoma kama ifuatavyo: “Mheshimiwa Samuel Sitta, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; salaam. Pendekezo la uteuzi wa jina kwa nafasi ya Waziri Mkuu. Ninafurahi kukuarifu kuwa, nimemteua Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda. Ninafurahi yaani Rais anasema, ninafurahi kukuarifu kuwa, nimemteua Mheshimiwa Mizengo, iliachwa Kayanza ninaiweka sasa Mizengo Kayanza Peter Pinda.

MBUNGE FULANI: Amepita huyo mia kwa mia. (*Makofi*)

SPIKA: Mbunge wa Mpanda Mashariki, kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nimefanya hivyo, kwa mujibu wa ibara ya 51(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Toleo la mwaka 1977. Kwa mujibu wa ibara hiyo ya Katiba, Waziri Mkuu, atashika madaraka hayo mpaka kwanza, uteuzi wake uthibitishwe na Bunge kwa Azimio litakaloungwa mkono na Wabunge walio wengi. Hivyo basi, ninakuletea jina la Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda kwako, kwa ajili ya hatua zipasazo kufanywa na Bunge letu Tukufu. (*Makofi*)

Ninakutakia wewe na Waheshimiwa Wabunge wote, kila la heri katika mwaka mpya wa 2008 na kazi njema. Wasalaam; Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri Muungano wa Tanzania.” (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, sasa tunaingia hatua ya tatu; nitamwomba Mwanasheria Mkuu wa Serikali, atoe maelezo ya utangulizi na baadaye kulisoma Azimio la Kumthibitisha Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda kuwa, Waziri Mkuu na kisha kumalizia kwa kusema anaomba kutoa hoja.

AZIMIO LA KUMTHIBITISHA WAZIRI MKUU

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa fursa hii uliyonipatia ya kuwasilisha hoja ya Serikali, kuliomba Bunge lako Tukufu limthibitishe Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliyeteuliwa na Mheshimiwa Rais, kwa mujibu wa ibara ya 51 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno ya hayo, ninapenda sasa niwarejeshe katika kutekeleza jukumu langu la Kikatiba la kuwasilisha hoja ya kuliomba Bunge, lithibitishe uteuzi wa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, uliofanywa na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, kama Waheshimiwa Wabunge watakavyokumbuka, Mheshimiwa Rais, ameridhia kujiuzulu kwa aliyekuwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa na hivyo kupelekea nafasi hiyo muhimu kuwa wazi. Ibara ya 51(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inaelekeza kumteua Mbunge wa kuchaguliwa kutoka katika Jimbo la Uchaguzi, anayetokana na chama cha siasa, chenye

Wabunge wengi zaidi Bungeni au kama hakuna chama cha siasa chenye Wabunge wengi zaidi, anayeelekeea kuungwa mkono na Wabunge walio wengi kuwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na kwamba, mtu atakayeteuliwa kushika wadhifa huo, hatashika madaraka hayo mpaka kwanza uteuzi wake uwe umethibitishwa na Bunge kwa Azimio litakaloungwa mkono na kura za Wabunge walio wengi hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kama ulivyolarifu Bunge lako hili Tukufu hivi punde, Mheshimiwa Rais, amemteua Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda ni Mbunge wa kuchaguliwa kutoka Jimbo la Uchaguzi la Mpanda Mashariki na anatoka Chama cha Mapinduzi, ambacho kwa mujibu wa matokeo ya Uchaguzi Mkuu uliofanyika tarehe 14 Desemba, 2005, yaliyotangazwa na Tume ya Uchaguzi, ndicho chama chenye Wabunge wengi zaidi humu Bungeni. Vilevile kwa mujibu kwa masharti ya 51(2) ya Katiba, Mheshimiwa Rais, amelileta jina la Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda katika Bunge hili Tukufu, kwa ajili ya kuthibitishwa.

Mheshimiwa Rais, amewasilisha jina la Mheshimiwa Mizengo Kanyanza Peter Pinda ili mlithibitishe kwa sababu anafaa na ana sifa zote hizo nilizozitaja hapo juu. Nikianza na suala uchapakazi; Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda siyo mgeni kwa Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla. Watu wengi ikiwa ni pamoja na Waheshimiwa Wabunge, wanafahamu uwezo wake wa kufanya kazi kwa muda mrefu bila kujali saa za kawaida za kufanya kazi. Wanaofahamu pia uwezo wake huo, wamejidhihirisha katika muda wote alioshika nyadhifa mbalimbali za uongozi wa umma, ndani ya Serikali na taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, watakulaliana nami kwamba, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda ni mtu mpole, mwadilifu, asiyekuwa na makuu, mwenye busara nyingi, hekima, msikivu wa hali ya juu na mchapa kazi hodari. Anapokumbana na tatizo lolote anashaurika na kuupokea ushauri kwa mikono miwili, lakini vilevile ana uwezo wa kuchambua na kupima hoja mbalimbali. Uwezo wake mpana na uelewa mambo katika kufikia maamuzi, umejidhihirisha katika utumishi wake wa umma ndani na nje ya Bunge hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunaziwasilisha sifa hizi kwenu ili sote kwa pamoja, tumthibitishe Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda ili aweze kuyabeba majukumu yote yanayoendana na wadhifa wa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwani anaweza kuyahimili.

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza hayo yote, sasa kwa unyenyekevu, heshima na taadhima, ninaliomba Bunge lako hili Tukufu, lithibitishe uteuzi wa Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge wa Ukanda wa Mashariki, uteuzi uliofanywa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili awe Waziri Mkuu, kwa kupitisha Azimio lifuatalo:-

Azimio la Bunge la Kumthibitisha Waziri Mkuu, chini ya ibara ya 51(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kanuni ya 55(2) ya Kanuni za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

KWA KUWA, kwa mujibu wa ibara ya 51(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais anapaswa kumteua Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ndani ya kipindi cha siku 14 tangu kuapishwa kwake kushika madaraka yake au baada ya nafasi ya Waziri Mkuu kuwa wazi kwa mujibu wa vipengele vya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

KWA KUWA, Chama cha Mapinduzi ndicho chama chenye Wabunge wengi zaidi kuliko Wabunge wa vyama vingine vilivyoapishwa Bungeni na hivyo, Rais anayo haki ya kumteua Waziri Mkuu, kutoka mionganoni mwa Wabunge waliochaguliwa katika majimbo ya uchaguzi mionganoni mwa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi;

KWA KUWA, Mheshimiwa Rais amemwarifu Mheshimiwa Spika kwamba, amemteua Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge wa Jimbo la Mpanda Mashariki, kuitia chama cha Mapinduzi kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Spika amewasilisha jina lake katika Bunge hili Tukufu;

KWA KUWA, uteuzi wa Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge wa Mpanda Mashariki, kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, umezingatia masharti yote ya ibara ya 51 ya Katiba ya Jamhuri ya Tanzania;

HIVYO BASI, Bunge hili katika mkutano wake wa kumi, lililokaa hapa Dodoma leo tarehe 8 Februari, 2008 linathibitisha uteuzi uliofanywa na Mheshimiwa Rais wa kumteua Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge wa Mpanda Mashariki, kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja hiyo imetolewa na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na imeungwa mkono; sasa nitaomba muiamue. Wale wanaotaka kuchangia, wasimame walipo ili niweze kuwatambua. Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani Bungeni.

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninaomba kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujaalia leo hii, nchi yetu baada kuwa katika *tension* kubwa, hatimaye Mheshimiwa Rais, katuletea jina la Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda kuwa, awe Waziri Mkuu wetu baada ya Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, kuomba ajiuzulu kutokana na kubeba majukumu ya kisiasa. Kwanza, ninapenda kuchukua nafasi hii, kumshukuru sana aliyekuwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, kwa kitendo cha kishujaa, cha kizalendo na hekima, kwa nia yake safi katika kuitumikia nchi yake na kuisaidia nchi yake na katika kumsaidia Rais katika majukumu yake ya Urais. Ameisadia sana nchi, amelisaidia sana

Bunge na amekisaidia pia chama chake, ninampongeza sana kwa tendo la kishujaaa alilolifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kiasi fulani, ninamfahamu Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, toka mwaka 1982, pale nilipopata bahati ya kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani, wakati ye ye akifanya kazi Ofisi ya Rais ni mchapakazi na mwadilifu. Sifa moja kubwa, baada ya kuingia Mfumo wa Vyama Vingi, amekuwa mtu wa kusimama katika haki. Sisi sote tumefarijika sana na uteuzi huo na ninawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote, kwanza, tumpongeze Mheshimiwa Rais, kwa kutuelewa vizuri na kuzikuna nyoyo za Wabunge na Watanzania, kwa kutuletea Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda. Ninawaomba Wananchi wote wa Tanzania, vyama vyote vya siasa na Wabunge wenzangu humu ndani ya Bunge, tumpe ushirikiano wa hali ya juu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda katika kufanikisha majukumu yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Bunge ni moja kati ya taasisi tatu muhimu katika nchi yetu. Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, amekaa katika Ofisi ya Waziri Mkuu, anaelewa kabisa nia yako safi na nia ya Wabunge, kuifanya taasisi hii ifanye kazi kwa uadilifu na kwa ufanisi, kwa mujibu wa Katiba yetu. Tunamwomba mara atakapoapishwa, ajue pia kwamba, ana jukumu la kuhakikisha taasisi hii inatimiza majukumu yake kikamilifu. Tatu, ninamwomba sana Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, kama Msimamizi Mkuu wa Shughuli za Serikali, hoja za Wabunge na mahusiano na Wabunge yatakuwa ni mambo muhimu sana kwake. Sote tulioko hapa, tuna lengo moja tu la kumwondoa Mtanzania katika dimbwi la umaskini na kuifanya Tanzania iondokane na ombo omba na rasilimali zake ziwafaidishe Watanzania. Hatuna nia nyingine hapa, tofauti zetu za kisiasa, tutaziacha pale ambapo tunaona maslahi ya kitaifa yako mbele na hilo tumewahakikishia kabisa, tutalisimamia kikamilifu. Kwa sababu hiyo, basi ninaomba niunge mkono kwa dhati kabisa uteuzi na ninaamini ninaunga mkono kwa niaba ya wenzangu wote waliomo ndani ya Bunge hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. EDWARD N. LOWASSA: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi hii na mimi nizungumzie hoja iliyoko mbele yetu. Kwanza, nijiunge na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, kwa kumpongeza Rais sana, kwa kugusa nyoyo zetu, kwa sababu amemchagua mtu ambaye anafanana na Bunge hili, analijua Bunge na anaijua nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimefarijika sana, niliposikia jina la Mheshimiwa Mizengo Kanyanza Peter Pinda, kwa sababu ninajua anaingia Waziri Mkuu, tunayefanana vizuri sana. Anaingia mtu ambaye ni mchapakazi kweli kweli, mzoefu, mkweli na kada wa Chama cha Mapinduzi. Nimefanya kazi na Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, kwa muda mrefu. Huyu ni mmoja wa Mawaziri anayeijua nchi yetu; Kaskazini, Kusini, Mashariki na Magharibi. Pia ni mtu ambaye kwa uzoefu wake, anajali sana maslahi ya wanyonge wa nchi yetu. Vilevile ni mtu ambaye hufanya kazi bila kujali muda, hata

usiku wa manane unamwamsha anafanya kazi. Ana uzoefu mkubwa sana wa Serikali na chama chetu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, Bunge limepata Waziri Mkuu mahiri na makini, ninawasihi kila mmoja wetu, amuunge mkono maana tumepata kiongozi bora na siyo bora kiongozi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ninapenda nizingatie jinsia, kwa hiyo, nitamalizia na wasemaji wawili tu; Mheshimiwa Getrude Mongella na Mheshimiwa Anna M. Abdallah. (*Makofi*)

MHE. BALOZI GETRUDE I. MONGELLA: Ahsante sana, Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ndugu zangu Wabunge wote, ninasimama hapa kwa heshima kubwa, kwanza, kukubali historia iliyoadikwa na Watanzania. Sisi ambao tunapita sehemu mbalimbali za Afrika, hiki tulichokifanya Tanzania ya leo ni kikubwa mno. Watu walio wengi sasa hivi tungakuwa ndani ya vita, lakini kwa busara za Watanzania na kwa kukomaa kwa Watanzania kisiasa hasa Wabunge, tumevuka salama. (*Makofi*)

Si hilo tu, kwa kuwa na viongozi walioandaliwa vizuri chini ya Uongozi wa Chama cha Mapinduzi, kazi nadhani ya Rais haikuwa nyepesi, si ajabu hajalala kipindi chote cha matatizo haya, lakini ametumia busara, hekima na upendo mkubwa kwa taifa letu, kwa kutuchagulia Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, kuwa Waziri Mkuu wa Nchi hii. Mimi ninamfahamu sana Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, alipokuwa Ikulu alituhudumia kwa unyenyekevu sisi tuliokuwa Mawaziri na Wajumbe wa Kamati Kuu na alifanya kazi chini ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Kufanya kazi chini ya mtu kama Baba wa Taifa, inanipa faraja ya kwamba, amejifunza mengi ambayo atayatumia katika kusimamia shughuli za nchi hii. (*Makofi*)

Ninapenda pia niungane na wenzangu, kumshukuru kwa dhati ndugu yetu, Waziri Mkuu aliyeachia ngazi; ni ushuja wa hali ya juu na kama hatutachukua hii kama kigezo kikubwa cha kukomaa kisiasa, tutakuwa hatumtendei haki. Kwa busara yake, ametufikisha katika historia hii tunayoiandika leo. Tuna majirani zetu ving'ang'anizi na leo watu wengi wanakufa, kwa sababu kuna watu ambao hawana busara ya kusema nafasi unayopewa ni dhamana na wakati wowote unapaswa kuiacha hata kama huna kosa. Kwa hiyo, ndugu yetu, Mheshimiwa Edward N. Lowassa, huondoki kwa sababu una mapungufu ya utendaji, unaondoka kwa sababu ya demokrasia na utendaji kazi mzuri na hasa chini ya misingi ya demokrasia ambayo tunaijenga. Utakuwa pamoja nasi na tutafanya kazi pamoja. Ninaomba kitu kimoja; kila mtu kwa dini yake amwombee Rais wetu na Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, ambaye anabeba jukumu kubwa. Vilevile tumwombee Mheshimiwa Edward N. Lowassa, ambaye anarudi kuimarisha safu za nyuma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo, kwa kweli ninataka kusema, nimefurahi sana kwamba, nchi yetu inaweza kukabiliana na dhoruba yejote na tukavuka salama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono uteuzi huu. (*Makofi*)

SPIKA: Wakati tunaendelea, nimebadili mawazo kidogo na haya mambo yamo ndani ya mamlaka yangu, kwa hiyo, hakuna lolote unaloweza kufanya ila kukubali tu. Imenibidi niongeze wengine wawili, kwa uwakilishi wa rika. Kwa hiyo, baada ya Mheshimiwa Anna M. Abdallah, nitamwomba Mheshimiwa Zitto Z. Kabwe aongee, Mbunge kijana kuliko sisi sote hapa, halafu tutamalizia na Mzee John S. Malecela. Waheshimiwa Wabunge, ulimi ulitereza kidogo; Mpanda na Urambo ni Wilaya ambazo zinapakana. K wa hiyo, nilipotamka jina la katikati la Mheshimiwa Pinda kule kwao Kusini wanasema Kayanza, sisi pale Urambo tunaita Kayanda, kwa hiyo, msione kama hii ilikuwa ni hali nyingine; ni furaha tu kupata mtu mzuri. Kwa hiyo, sasa nitamwita Mheshimiwa Anna M. Abdallah. (*Makofi*)

MHE. ANNA M. ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami nijiunge na wasemaji walionitangulia katika kumpongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwanza kwa kukubali kujiuzulu kwa ndugu yetu mpenzi, Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa. Kuna baadhi ya watu walikuwa wana wasiwasi atakubali kweli? Lakini kwa busara yake, kwa jinsi mambo yalivyotokea, tunamshukuru kwamba amekubali lakini nimpongeze sana mwenyewe Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nadhani amefungua ukurasa katika kitabu cha Tanzania na ni matumaini yangu kuwa wengi tutapata darasa kutoka kwake, amefanya mambo ya kiutu uzima, ya kiukomavu, yenyenjibu tele na hekima tele, tunampongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nadhani kwa niaba ya Wabunge tutaendelea kumheshimu hata kama akiwa huku *back bencher*, heshima yake itabaki pale pale. Katika maisha ya binadamu unawenza ukatenda mazuri wengine wasiyaone kama ni mazuri, unawenza kutenda mabaya wengine wakaona ni mazuri tu bila kujali lakini katika maisha ya binadamu yeye amepitia nyadhifa nyingi amefika mpaka Waziri Mkuu lakini yeye bado ni Mbunge mwenzetu na ni Mbunge wa Jimbo lake la uchaguzi la Monduli, tutakuwa naye humu, tutavuna busara zake na nina hakika kama kutatokea wakati humu ndani ya Bunge pengine tunayumba, atatusaidia kutoa maoni yake, tunakushukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, labda kabla sijamuacha Mheshimiwa Edward Lowassa, naomba nimpongeze sana mama Regina Lowassa. Wakati kindumbwendubwe chote cha jana, maneno yote, mama Lowassa alikuwepo hapa anasikiliza, ni ujasiri mkubwa. Tunaomba wanawake muwe wajasiri. Mimi nina hakika alikuja, kwanza, kumpa tafu mumewe lakini alikuja kumpa tafu Waziri Mkuu. Ni mwanachama mzuri wa Umoja wa Wanawake na mimi ninamwomba kwamba katika kipindi hiki anachokipitia Mheshimiwa Edward Lowassa basi yeye atakuwa pamoja naye bega kwa bega. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nasema haya kwa kuwa mimi ni Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake wa Tanzania wa *UWT*. Ukiona mwanamke jasiri namna ile basi ujue anatokana na *UWT*, tunampongeza sana. Alichagua yeye lakini alichagua mwanamke imara, tunamshukuru sana, ingekuwa wengine sijui ingekuwaje hata kuteremka ngazi ...

SPIKA: Mheshimiwa Anna Abdallah, nakuomba uende kwenye hoja.

MHE. ANNA M. ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza nimsifie yeye mwenyewe kabla sijaenda kwenye hoja ili watu waelewe huko tunakotokea.

Mheshimiwa Spika, nataka niseme hivi, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Pinda, hajachupia ndani ya Bunge, hajachupia ndani ya uongozi, hajachupia kwenye Chama cha Mapinduzi ameanzia chini. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, maana tuna watu wengine wametokea kama chura ndani ya bwawa, siyo Mheshimiwa Mizengo Kayanza Pinda. Anakijua Chama cha Mapinduzi, anaijua *TANU* na *AFRO* kwa sababu yeye ndiye alikuwa msaidizi wa Mwalimu mpaka vyama hivi vinaungana mpaka tuko kwenye CCM. Mheshimiwa Mizengo Kayanza Pinda, ni mwanasiasa aliyekomaa. Inawezekana alikuwa hajapata vyeo vikubwa sana vya kichama lakini ndani ya Chama, amekomaa tumepata kada. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Bunge, yeye ameanza kuwa Mbunge wa kawaida, akapanda ngazi, akawa Naibu Waziri mpaka amekuwa Waziri wa Nchi mpaka leo. Ninawaomba wenzangu tumthibitishe kwa kura zetu zote awe Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mheshimiwa Mizengo Kayanza Pinda, ni mzoefu, mkweli, hana makuu, mpole, hana makundi, msikivu, anaijua Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nadhani tumshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mimi nimuunge mkono Mheshimiwa Hamad Rashid na Mheshimiwa Edward Lowassa kwamba Rais ametukonga nyoyo zetu.

Nimalizie kwa kuwaomba Wabunge wote kwa sifa hizi tulizozisikia kwa pande zote mbili hata kama ni upande wa Upinzani na upande wa Chama Tawala wa CCM, tunpe kura zetu zote na tukishamaliza hapo tunpe ushirikiano. Nina hakika Mheshimiwa Mizengo Kayanza Pinda atatusaidia katika kutuunganisha wote na kutokana na tabia yake, hatatugawa, atatuunganisha, tunpe ushirikiano, tumtakie kila la kheri. Najua hatujampa kura lakini natunguliza kumpa na kumtakia kila la kheri na Mwenyezi Mungu amzidishie nguvu ili aifanye kazi hiyo iliyoko mbele yake kwa nguvu zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kihistoria kabisa ya kuweza kuchangia machache kuhusiana na pendekexo ambalo Mheshimiwa Rais amelileta kwetu sisi Wabunge kwa mara nyingine

tena ndani ya kipindi chake cha kwanza cha uongozi ili tuweze kumpa msaidizi wake Mkuu, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ninayo machache sana, ni mambo matatu tu. La kwanza, ni suala la Katiba, *constitutionalism*. Kama jinsi ambavyo Mheshimiwa Rais wa Bunge la Afrika ametoka kuzungumza muda mfupi uliopita ya kwamba hali kama hii ingekuwa kwenye Mataifa mengine ya Afrika, sasa hivi tungekuwa kwenye *crisis* kubwa sana. Lakini tumepata *challenge* ya Kikatiba na ni ya muda ambao unatakiwa Kikatiba, Rais ametuletea jina la mtu ambaye anatuomba tuweze kumthibitisha na kuwa Waziri Mkuu na vile vile kiongozi wa shughuli za Serikali Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, suala hili ni la kihistoria kwamba tunai-*taste* Katiba yetu na imekuwa *tasted* na nchi na *institutions* zipo imara na kuanzia kesho *life goes on*. Sidhani kama itakuwa ni kawaida kwa sababu tuna kiongozi mpya lakini ninaamini kabisa kwamba misingi imara ya Taifa letu ambayo iliwekwa na waasisi wetu, itaweza kuendelezwa na kuwa imara zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, siwezi kusema kwamba nimewahi kufanya kazi na Mheshimiwa Mizengo Kayanza Pinda, kwa mara ya kwanza, nimekutana naye hapa Bungeni lakini nilibahati kwa siku chache za mwanzo kabisa wakati Mheshimiwa Mizengo Kayanza Pinda ameteuliwa kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Serikali za Mitaa, kushughulika naye kwa suala ambalo ni la kihistoria kabisa katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kulitokea tatizo kule Kigoma katika Manispaa ya Kigoma Ujiji, mara baada ya uchaguzi, idadi ya Madiwani wa Chama cha Mapinduzi na idadi ya Madiwani wa Chama cha CHADEMA ilikuwa *ime-tie up*, kumi kwa kumi. Tulikuwa tunatakiwa kuchagua Meya wa Manispaa ya Kigoma, kulikuwa na matatizo mlisikia baadhi ya Madiwani ilibidi watoroshwe ili kura ziweze kupungua lakini haikuwezekana kwa uimara wa Wabunge mahiri kabisa wa Viti Maalum wa CHADEMA wakamkamata Diwani yule *Air Port Dar es Salaam*. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Kabwe Zitto turudi, mnajua ni kuunga mkono hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Spika, ndio naenda huko, ahsante sana.

SPIKA: Njia yako ya kufika huko, ninaiona ndefu sana.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Spika, kwa kweli ilikuwa ni *crisis* lakini tukakutana na Mheshimiwa Mizengo Kayanza Pinda, tukakaa Kigoma kwa takriban siku tatu tukajadiliana na tukakubaliana kuunda Manispaa ya pamoja kati ya Chama cha Mapinduzi na Chama cha CHADEMA kwa makubaliano maalum ambayo baadaye kwa juhudhi za Mheshimiwa Mizengo Kayanza Pinda, makubaliano yale yakafanywa kuwa ni sehemu ya marekebisho ya Sheria za Serikali za Mitaa ambazo tulizipitisha hapa Bungeni mwezi Novemba mwaka jana. Kwa hiyo, hii inadhihirisha sifa

yake Mheshimiwa Mizengo Kayanza Pinda ya kuwa *fair* lakini pia ya kusikiliza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa yako tu ni kwamba mwezi wa tano mwaka huu 2008, Chama cha CHADEMA kinakabidhi rasmi Umeya kwa Chama cha Mapinduzi, kwa sababu makubaliano yale yalikuwa ni kuongoza nusu kwa nusu, sisi nusu yetu tunamaliza mwezi Mei. Ninaamini kabisa kwa kuwa Mheshimiwa Mizengo Kayanza Pinda, ndio aliyejewa *Principal Architect* kwa kushirikiana nasi katika muafaka ule, atakuwepo Kigoma akishuhudia tukikabidhi Umeya kwa Chama cha Mapinduzi ili nao pia wamalizie ungwe yao ya mwisho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hilo, inaonyesha kabisa kwamba moyo huo wa ushirikiano na wa kusikiliza, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Pinda, atauendeleza katika Bunge hili. Kama alivyosema Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, sisi Kambi ya Upinzani, tutampa ushirikiano wote anaouhitaji ili kuweza kuliongoza Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, nami pia ninaungana na wengine wote waliotangulia kuunga mkono hoja ya pendekezo la Mheshimiwa Rais la kumteua Mheshimiwa Mizengo Kayanza Pinda, kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, msemajji wangu wa mwisho kwa hoja hii, ni Mheshimiwa John Malecela, Mbunge wa Mtera.

MHE. JOHN S. MALECELA: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, ninapenda kuchukua nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii *last but not least* ya kuweza kuchangia katika hoja ya kuunga mkono uteuzi wa mwenzetu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Mizengo Pinda, kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungao wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kwako wewe. Jana hali ilivyokuwa hapa, mimi nasema na ninawaomba wenzangu tukushukuru sana kwa busara zako ambazo ziliweza kutuongoza ingawa mambo yalianza kuwa magumu lakini baadaye tukayamaliza vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pili, ninapenda kuchukua nafasi hii ya kumpongeza mwenzetu, kijana wangu, Edward Ngoyai Lowassa, Mheshimiwa Waziri Mkuu, ambaye alijiuzulu jana.

Ndugu zangu mnisamehe kidogo, katika Bunge hili niseme moja au mawili ya kifalsafa kuhusu Tanzania. Kifalsafa, katika karne ya 16 na 17 kulikuwa na matatizo katika nchi nyingi hasa za Ulaya, kulikuwa na swal, hivi madaraka ya kuendesha

Serikali za wananchi mtu anarithi, ya nguvu au yanatoka wapi? Wengine wakasema wao wanapewa moja kwa moja na Mungu kwa hiyo ni Wafalme wakishasema wamesema. Wengine wakasema hapana madaraka hayo yanatoka kwa Mungu yanapitia kwa wanadamu halafu ndio yanakuja kwa mwanadamu anayempenda na ndio likaja lile neno sauti ya wengi ni sauti ya nani?

WABUNGE FULANI: Ya Mungu.

MHE. JOHN S. MALECELÀ: Kwamba Mungu anawatumia wanadamu wakupe wewe madaraka basi ingawaje yametoka kwa Mungu lakini yamepitia kwa wananchi, kwa hiyo lazima uwaheshimu.

Mheshimiwa Spika, tatu, kwa hiyo, nataka niseme, sisi Tanzania nchi yetu imeendelea kuwa ya amani, kama nchi yetu imeendelea kuwa ya utulivu, ni kwa sababu Watanzania kwanza jambo moja ambalo tumelisisitiza ni madaraka yote tuliyonayo na sisi wote Wabunge hapa yanatokana na Watanzania wenyewe na ndio sababu hata katika Katiba yetu tukayaweka kwamba madaraka ya Serikali yeoyote Tanzania yanatokana na wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nne, nataka nimshukuru sana Rais wetu mpandwa, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa hekima zake kwamba baada ya yote haya lakini ametuteulia mwenzetu ambaye sifa zake zimesomwa hapo na kwamba sifa hizo ni kweli anastahili ili achukue madaraka ya kuendesha nchi hii.

Mheshimiwa Spika, sisi Wabunge wote hapa ni kama wajenzi angalieni *mapyramid* ya Misri, hayakujengwa siku moja, yalijengwa kwa miaka. Kwa hiyo, kila mtu anaweka tofali lile analoliweza na kuwaachia wengine kuja kuendelea na ujenzi huu.

Mheshimiwa Spika, kwa mwenzetu aliyeteuliwa leo, sisi Wabunge, tuna jukumu moja la kuwaonyesha Watanzania kwamba kama ni suala la umoja, kama ni suala la wote kuitikia kwa kitu kimoja lianzie hapa leo kwa kumpa mwenzetu kura zote na baada ya hapo liende kwa wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, nataka niseme kwamba Wabunge wenzangu tukumbuke kila siku kwamba nchi ndio yenyе maslahi ya kudumu ningetumia lugha ya kigeni, *Tanzania has permanent interest*, sisi Wabunge tutakuja na tutaondoka, watakuja Wabunge wengine lakini Tanzania na Watanzania watakuwepo kila wakati, tuhakikishe kwa kuungana pamoja kwamba Watanzania hawa tunawaondoa katika dimbwi la umaskini na tunawapunguzia baadhi ya matatizo waliyonayo. Nina hakika kwa kiongozi tuliyepewa na ambaye hivi sasa nikimaliza tu tutampitisha, lazima kazi hiyo tuifanye kwa ufanisi sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, nataka niungane na wenzangu kwa kuunga mkono hoja iliyoko mbele yetu. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja iliyo mbele yetu ni ya aina yake ambayo haihitaji majumuisho, kwa hiyo sitamwita Mheshimiwa mtoa hoja, Mwanasheria Mkuu kwa sababu hakuna cha kujibu hapa.

La pili, kura zake siyo za sauti ni za siri, ndio Katiba inavyotuhitaji hivyo. Kwa hiyo, Katibu sasa gawa karatasi za kupiga kura.

WABUNGE FULANI: Haombi?

SPIKA: Nimeruka hapo, namwomba sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu Mteule, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, aje aongee nasi. Karibu sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Makofi/Vigelegele*)

MHE. MIZENGO K. P. PINDA – WAZIRI MKUU MTEULE: Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, nimepewa fursa hii kama alivyoelekeza Mheshimiwa Spika, nijaribu kusema mambo machache kabla hamjafanya uamuzi wenu wa mwisho wa kunithibitisha.

Mheshimiwa Spika, nimepata tabu kidogo, lakini naomba nitangulize shukrani zangu za dhati kwa namna ambavyo mlipokea uamuzi wa Rais. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi ni mtoto wa mkulima na katika familia yetu, ni mtoto wa kwanza, kwa hiyo nafasi hii niliyopewa na Mheshimiwa Rais kidogo ni nzito na nina hakika hata wazee nyumbani waliposikia watakuwa wameshtuka kweli kweli na usiri uliokuwepo ni mkubwa, taarifa hii nimeipata mchana huu huu, nikamwambia Rais nitajitahidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kitaaluma, mimi ni Mwanasheria kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Nimefanya kazi na Mheshimiwa Andrew Chenge, kaka yangu hapa kwa muda wa miaka kama minne tu hivi, kuanzia mwaka 1974 mpaka mwaka 1978, nilipokuwa nimemaliza Chuo Kikuu, amenilea vizuri sana Mheshimiwa Andrew Chenge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, nikaitwa Ikulu, siku hiyo nilikuwa mbali kabisa Songea, nikalazimika kurudi. Nikaambiya Rais anaomba uje umsaidie kufanya naye kazi kwenye *private* ofisi yake chini ya usimamizi na uongozi wa Mheshimiwa Butiku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimekuwa mtumishi wa Ikulu pale katika nafasi mbalimbali ingawa kwa sehemu kubwa nilikuwa Katibu wa Rais Msaidizi tangu wakati wa Mwalimu kwa miaka saba.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, nikawa na Mheshimiwa Mzee Mwinyi kwa miaka yake yote kumi. Kati ya 1995/2000, nilikuwa na Mheshimiwa Rais Mstaafu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kufanya kazi Ikulu, ni jambo zito, si dogo lakini nilijifunza kufanya kazi kulingana na nidhamu ya Ikulu ilivyo. Si mwanasiasa kwa maneno mengine

kama uanasiasa basi nimejifunza kutokana na kukaa karibu na yale maua waridi, haswa Waswahili wanasema ukikaa karibu na ua waridi unanukianukia waridi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwaka 1995, nilitama kubadili nyanja nikajaribu lakini mambo hayakwenda vizuri. Sikukata tama, mwaka 2000, nikajaribu tena lakini nilipokuwa najaribu huu ulikuwa ni wakati sasa ambapo nimekutana na Rais Benjamin William Mkapa, Mzee Lumbanga akasema ngoja kwanza nimuulize Rais wangu. Alipomuuliza Rais, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, akasema Pinda utaweza kazi hiyo? Ubunge kuna mambo mengi, mengine hutayaweza, hapa ndio mahali kwako. Nikamwambia, hapana Mzee, nimeombwa sana. Akasema basi nenda, kikubwa ukishindwa rudi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri mwaka 2000, sikurudi Ikulu wananchi wakaamua kunichagua kwa kauli nzito tu na ndio ukawa mwanzo wa kuungana sasa na Wabunge ambaa baadhi yao ni uanasiasa wa siku nyingi sana. Mwaka 2005, nikajaribu tena na nikaungwa mkono na wananchi wa Jimbo langu vizuri sana.

Kwa hiyo, kama ni uanasiasa, Waheshimiwa Wabunge wenzangu, ni hicho kipindi kifupi cha miaka saba lakini naomba niseme ukifanya kazi ndani ya Ofisi ya Rais au ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu katika sekta hii inaitwa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa hata ungekuwa nani uthalazimika kukomaa tu huna ujanja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimejifunza mengi kupitia kwa viongozi waliokuwepo wakati huo, Mheshimiwa Ngwilizi lakini kubwa zaidi ni Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati huo pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu hivi sasa ambaye amejiuzulu hivi karibuni. Viongozi hawa ninaweza nikasema kwa ufupi kama yako mambo mnayaona pengine mazuri juu yangu, ni hawa viongozi ndio wamenilea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, najua utanipa nafasi mwishoni endapo Waheshimiwa Wabunge watakubali kunithhibitisha ili niweze kutoa maelezo mafupi ya shukrani, lakini sina budi kumshukuru sana Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Lowassa, ndani ya kipindi kifupi hiki amenikomaza sana. Ni kiongozi mmoja mzuri sana kwa maana ya utendaji kazi lakini nilimfurahia sana kwa sababu ameniwezesha kila ninapajaribu kusema nanyi Waheshimiwa Wabunge, mnaona faraja lakini kwa kweli nyuma yake kwa miaka hii miwili kama Waziri wa Nchi, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, aliyekuwa anafanya msukumo mkubwa ni yeye. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, katika kuwaomba kama mtaona inapendeza kunithhibitisha ili kuweza kukidhi takwa la Rais na la Katiba ya nchi yetu, basi naomba mazingira haya yote yalijonisababishia nifanane na mnavyoniona kwa sehemu kubwa yamejengwa na haya maelezo niliyowapa. Mkiweza kunithhibitisha, ninaomba niwaahidi tu nitakachokuwa nimekiona kipyaa ni haya madaraka sasa ambayo naona yako mbele

yangu lakini kwa maana ya Mbunge mwenzenu, kwa maana ya Pinda yule tulyemzoea, atabakia kuwa ni yule yule. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitajitahidi sana kuendelea kushirikiana na Mawaziri watakaokuwa wamepewa fursa ya kuungana nami na Manaibu Mawaziri kwa ujumla wao, mtajenga uhusiano mkubwa zaidi ndani ya Bunge hili kwa pamoja, pamoja na Waheshimiwa Mawaziri wenzangu. Makubwa ambayo baadhi ya wasemaji wameyasema ni kujaribu kwa dhati kabisa kujenga Bunge moja hasa katika suala au masuala yanayohusu maslahi ya Taifa letu.

Katika hilo Waheshimiwa Wabunge, mimi tamaa yangu ni kufanana kama wenzetu wakubwa walipofikia. Ukienda Israel, Marekani, Uingereza pamoja na tofauti zao za vyama mbalimbali lakini katika masuala ya msingi ya maendeleo wako pamoja.

Nitajitahidi endapo mtaridhia ombi la Rais la kutaka nimsaidie lakini kwa ujumla nimsaidie zaidi hapa ndani ya Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache ingawa hukuniambia kwamba niombe na wakati mwingine unapata taabu sana kuomba jambo kama hili

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu mteule imetosha!

MHE. MIZENGO KAYANZA PETER PINDA: Lakini nataka niseme asanteni sana na kama mtaona itafaa basi tumsaidie Rais kuweza kutimiza majukumu yake ya kikatiba. Nawashukuru sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana! Kwa kweli ujumbe wa namna hii inabidi Spika asimame tu, kwa kweli nimeguswa sana na hotuba hiyo Mheshimiwa Waziri Mkuu mteule, kwa kweli ni mwanzo mzuri. Kwa hiyo, jamani ndiyo hivyo tena mia kwa mia. (*Kicheko*)

Wale mnaohesabu basi tuwahesabu Waheshimiwa Wabunge. Aaah! Kumbe utaratibu ni kengele sijui nani atakuwa bado kwenye chai? Lakini ndiyo utaratibu kwa dakika tano hizi kengele wakati huo mnaanza kuhesabu na vijana wa kuhesabu mwendee!

Wapo wangapi?

MBUNGE FULANI: Wanane!

SPIKA: Kwa kila *section* wagawie kazi. Hawa wote ni wafanyakazi wa Ofisi ya Bunge, kwa hiyo, siyo watu wageni hapa.

KATIBU: Ndiyo wanagawa karatasi za kupigia kura.

SPIKA: Aaaah! Mmenihesabu na mimi? (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge ndani ya Ukumbi huu tupo 281, unaweka V kwenye Ndiyo. Wote tumepata karatasi za kura?

WAHESHIMIWA WABUNGE: Bado!

SPIKA: Haya vijana onyesheni sasa masanduku ya kura ili Waheshimiwa Wabunge wayaone.

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo masanduku ya kukusanya kura zetu, kila mmoja wetu amepiga kura?

WAHESHIMIWA WABUNGE: Ndiyo!

SPIKA: Tayari! Basi kusanyeni sasa kura na walihitajika mashahidi wawili, kwa hiyo, kwa sababu huu ni uchaguzi namteua Mheshimiwa Said Nkumba na Mheshimiwa Fatma A. Fereji waende wakashuhudie kuhesabu kura. (*Makofi*)

Vijana kusanyeni kura! Basi sidhani kama itachukua muda lakini tuendelee kunong'ona taratibu na polepole na baada ya dakika chache tutatoa matokeo.

Waheshimiwa Wabunge, hiki bado ni Kikao cha Bunge, napenda kuwakumbusha Kanuni ya 66 kuhusu staha ndani ya Bunge, Kanuni ndogo ya 3(b). Nanukuu: "Mbunge aliyepo Bungeni wakati huu atatakiwa kutulia na kukaa kwa heshima mahali pake na hatatangatanga kwenye ukumbi wa mikutano bila sababu." Nawaona baadhi yenu mnakaribia kuathiri Kanuni hii, mnatangatanga humu sijui mnatafuta nini! (*Kicheko*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, matokeo ya kura zetu ni kama ifuatavyo:-

Jumla ya kura zote zilizopigwa ni 282, nadhani kuna mmoja aliongezeka, Naibu Waziri wa Elimu ya Juu aliingia ndani. Kwa hiyo, siyo 281, ni 282, kura iliyoharibika ni moja, kura za hapana ni mbili, ajabu kweli!! Kura za ndiyo ni 279. (*Makofi*)

Ushindi huu ni wa kiwango cha asilimia 98.9. Kwa hiyo kwa mujibu wa Katiba ya nchi yetu hususan kifungu kile cha 51(2) inayo furaha kumtangaza Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda kwamba amethibitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano kuwa Waziri Mkuu. (*Makofi*)

Sasa Waheshimiwa Wabunge kwa heshima na taadhima namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu Mteule aweze kuzungumza nasi. Karibu Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Makofi*)

MHE. MIZENGO KAYANZA PETER PINDA - WAZIRI MKUU MTEULE: Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwanza naomba kabisa nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuwepo hapa Bungeni jioni hii na kuweza kufanya kazi ambayo mimi nitaienzi sana kwa kipindi kile nitakachopewa fursa ya kumsaidia Rais wetu.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa dhati kabisa nimshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa heshima kubwa sana aliyonipa ya kuniamini na hatimaye kupendekeza jina langu mbele ya Bunge langu Tukufu. Hii ni heshima kubwa sana kwangu na ni deni kubwa sana kwa upande wangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mitajitahidi kufanya kila litakalowezekana kutimiza majukumu yangu ili kuweza kwenda sambamba na azma ya Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wakati natoa maelezo nilitumia dakika kidogo kumshukuru Mheshimiwa Edward Lowassa, Mbunge, aliyekuwa Waziri Mkuu tangu tulipoingia kwenye Awamu hii ya Nne ya Serikali, naomba nirudie kumshukuru tena. (*Makofi*)

Uamuzi wake kwangu mimi ni mafunzo makubwa, lakini naamini hata kwa viongozi wote waliomo humu ni jambo la mfano ambalo kila mmoja wetu anapaswa kulitafakari na kwa hakika inapofikia hatua kama hiyo kukubali kufanya kama alivyofanya. Mimi naamini ataendelea kuwa kiongozi wetu kwa kadri itakavyowezekana.

Lakini naamini vilevile ataendelea kuwa ni mwenzetu ndani ya Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ataendelea kuwatumikia wananchi wake wa Jimbo la Monduli, kama ambavyo amekuwa akifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge wenzangu ni kweli nimeva kiatu cha Mheshimiwa Lowassa, lakini sina hakika kama kitanienea. Amekuwa ni msukumaji wa mambo mazito na wengi tunajua mfano mzuri kwa upande wa elimu. Lakini nitajitahidi kienee. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilimshukuru Mheshimiwa Brigedia Jenerali Mstaafu Ngwilizi, narudia kumshukuru sana. Namshukuru yeye, nawashukuru sana Makatibu Wakuu ambao nimefanya kazi nao wakati nikiwa Naibu Waziri na hivi sasa nikiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu. Nawashukuru na wataalam wangu wote ambao kwa pamoja tulishirikiana vizuri sana na hawa walinijengea uwezo mkubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru wewe mwenyewe kwa kunipa fursa hii adimu. Ni muda mfupi nitakuwepo hapa mbele yako, lakini ni muda mzito kwa kuwa sasa kupitia Bunge lako Tukufu mmetekeleza jukumu lenu zito na kwa maana hiyo hiyo mmenipa kazi ya kufanya ndani ya Bunge hili. Nakushukuru sana wewe mwenyewe, Naibu Spika na Wenyeviti wako wote ambao kwa kawaida wanakusaidia unapokuwa na majukumu mengine. Nimepata ushirikiano wao wakati nikiwa bado Naibu Waziri katika nyakati tofauti, naamini tutaendelea kufanya kazi nao vizuri na wewe mwenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, yapo mambo mengi ambayo unapokuwa Bungeni hapa unajifunza. Moja ya jambo ambalo naomba niseme, nilipoingia Bungeni kwa mara ya kwanza nilishangaa sana kwamba pamoja na kwamba walikuwepo Wabunge wa miaka mingi lakini ndani ya kipindi kifupi cha siku moja, mbili nilionna ni kama nafanana nao. Hii inaonyesha *potential* iliyopo kubwa sana ya kuweza kujenga undugu, mahusiano mema, kuheshimiana na kwa uhakika kuweza kufanya kazi zetu kwa pamoja kwa namna ambayo wananchi wanatarajia tufanye. Natamani sana hali hiyo iendelee na kwa kweli tuimarishe zaidi kwa pamoja naamini ni msingi muhimu sana katika kuendesha shughuli zetu ndani ya Bunge hili. (*Makofī*)

Mheshimiwa Spika, Kamati Teule imefanya kazi yake na ndiyo iliyopelekea mimi pengine kuwepo hapa leo. Sisemi nawashukuru kwa kuwa nimefikia hatua hii ya kuwa Waziri Mkuu mteule, la hasha, kwa sababu najua nimepewa kazi nzito ambayo itabidi kuifanya. Lakini nilichokiona kikubwa kwangu mimi kama mwenzenu ambaye tutakuwa pamoja ndani ya jahazi hili, ni kukubali kwamba katika utendaji wetu wa kazi ndani ya Serikali lazima tujitahidi kufanya kazi hiyo vizuri. Ni lazima wale wanaotusaidia hasa kwa upande wa Mawaziri na Makatibu Wakuu tuhakikishe wanatekeleza majukumu yao inavyotakiwa. Ni lazima tujitahidi wasaidizi wetu hawa watupe ushauri wa kweli, ushauri makini ambaeo yake ni yale ya kujenga Taifa letu. (*Makofī*)

Mheshimiwa Spika, kwa kifupi niliposikiliza mambo mengi yaliyokuwemo kwenye taarifa hii ni kama vile walikuwa wananiambia Mheshimiwa Pinda, ukibahatika kuwepo hapo basi jitahidini kuhakikisha dalili zozote za maovu ndani ya utendaji wa Serikali zinasimamiwa na kudhibitiwa kikamilifu.

Jukumu hili ni letu wote Wabunge kwa ujumla, sisi ambaeo tutapata bahati ya kumsaidia Rais wetu kwa karibu, lakini vilevile wananchi kwa ujumla wao. Sidhani kwamba kutokana na yaliyojitokeza ndani ya taarifa hiyo mtataka tuendelee kutaka kujua kipi kingine bado na kipi tunatakiwa tukifanyie nini. Kwangu mimi kama kiongozi mtarajiwu, ni kuona *in a positive way* ili yale ambayo yanajitokeza kama mapungufu kwa dhati kabisa tuweze kuyasimamia vizuri. (*Makofī*)

Mheshimiwa Spika, katika mjadala uliokuwepo Bungeni yamesemwa mengi juu ya vyombo vyetu mbalimbali vyatolye. Nadhani kubwa ni kupokea hiyo rai tuliyoiptata kutoka kwenye Kamati Teule, kama Serikali tuyafanyie kazi ya ziada, kama Serikali tuone kama kuna maeneo yenye mapungufu tujaribu kuyafanya marekebisho yanayostahili TAKUKURU, Polisi, Idaraya Usalama wa Taifa na vyombo vingine vyote ambavyo kazi yao kubwa ni kuisaidia Serikali kuweza kusimamia vizuri utendaji ndani ya Serikali. (*Makofī*)

Mheshimiwa Spika, naamini kwa dhati kabisa kwamba, kama haya tutayatazama kwa mtazamo wa kwenda mbele yapo mabadiliko ya dhati yatakayotuwezesha kuwapa wananchi matarajio na matumaini yaliyo ya uhakika zaidi katika utendaji wetu na usimamizi wa majukumu yaliyo mbele yetu. (*Makofī*)

Mheshimiwa Spika, Waziri Mkuu kwa mujibu wa Katiba ni Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni, lakini najua vilevile kwamba Bunge nalo lina eneo lake la utendaji katika utumishi wetu wa Serikali. Hamu yangu kubwa ni kuona kwamba maeneo haya yote mawili, lile nitakalolisimamia na hili ambalo linasimamiwa na na Mheshimiwa Spika yote yanafanya kazi kwa lengo moja la kuwahudumia wananchi kama inavyotakiwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nitajitahidi kufanya ushirikiano kwako, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Kamati na Waheshimiwa Wabunge wote na nitawaomba na wenzangu tutakaoteuliwa kumsaidia Rais tufanye hivyo. Mimi naamini kwa dhati kabisa tukijenga msingi huo Bunge hili tunaweza kabisa kutimiza wajibu wetu kwa pamoja kwa kadri ambavyo tumedhamiria. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Bunge hili ni Bunge ambalo linakidhi mahitaji ya Katiba yetu ya mfumo wa Vyama Vingi. Mimi naelewa kwamba wakati mwingine eneo hili linawezwa kuwa gumu kama hamkuwa makini, lakini mimi naamini kabisa kama lengo letu ni moja, kama lengo letu ni kuwasaidia wananchi, kama lengo letu kwa ujumla wake ni kutaka kuleta maisha bora kwa kila Mtanzania, hoja haiwezi kuwa Vyama Vingi, hoja kubwa mbele yetu ni Wabunge tuliomo humu ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuyafanya hayo ambayo wananchi wanategemea tuyafanye. Nitajitahidi kwa kadri ya uwezo wangu na kwa kuamini kwamba nitapata ushirikiano wa kutosha, tujaribu kuleta hiyo hali ambayo ina mwelekeo wa kujibu yale ambayo wananchi wanataka tuwafanyie. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nimekuwa katika Bunge lako Tukufu kwa vipindi viwili tofauti lakini naomba nichukue fursa hii kwa dhati kuwashukuruni sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu, viongozi wote ambaa mmekuwa pamoja nasi katika vipindi hivyo viwili kwa namna ambavyo mmesaidia sana wengine tulipokuwa bado wadogo kutuelimisha, kutufunza na kwa kweli kutujengea uwezo ambaa leo tunatamani tuuone katika nyanja mbalimbali. Waheshimiwa Wabunge wenzangu mimi nawashukuruni sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi, naomba nitoe wito kwa Watanzania wenzangu popote pale walipo hapa Tanzania tushirikiane, tufichue maovu yote kwa lengo la kusaidia nchi yetu. Kwani kazi hiyo si ya mtu mmoja, ni kazi yetu sisi wote. Narudia katika kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi natoa wito kwa Watanzania wote popote pale walipo tushirikiane, tufichue maovu kwa kadri itakavyowezekana katika ngazi zote mbili ndani ya Serikali za Mitaa na hata ndani ya Serikali yenyewe pale yatakapo jidhahirisha.

Mheshimiwa Spika, naomba nivishukuru sana vyombo vyahabari, mimi nawafahamu tangu nikiwa Naibu Waziri. Vyombo hivi vinasaidia sana katika kutoa habari kwa Watanzania. Nitajitahidi kufanya nao kazi kwa karibu na kwa imani moja tu kwamba taarifa watakazajaribu kuzitoa kwa ajili ya wananchi wetu wa Tanzania ni taarifa za kweli, zenye kina, ambazo si za uzushi na hazina nia yoyote mbaya katika utoaji wa habari ambazo zinahitajika kwa matumizi ya Watanzania wetu. Vyombo hivi

ni muhimu sana na hatuna budi kuvisaidia viweze kutimiza wajibu wake inavyotakiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi ya mwisho kuwashukuru sana wazazi wangu. Baba yuko hai na umri wake ni miaka themanini na moja. Mama yuko hai na umri wake ni miaka sabini na tisa. Nawashukuru kwa sababu naamini watakuwa wamefanya kazi nzuri, walijitahidi kunilea vizuri na pengine kwa makuzi ya maisha ya vijijini, wamenifanya nikafanana na kile ambacho pengine Taifa linataka. Kwa kifupi namshukuru sana Mwenyezi Mungu kunipa wazazi hawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya kwa sababu mambo haya huwa hayaotwi, sidhani kama wataweza kupata fursa ya kuwahi kuja kuona hatua ya mwisho ya kazi kubwa mliyoifanya leo kwa maana ya kiapo. Lakini kuitia Bunge lako Tukufu, narudia kuwaambia ahsanteni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niishukuru sana familia yangu, bahati mbaya Mama Pinda hakupata nafasi lakini ameshakuja Dodoma, lakini kwa sababu hatukuwa na ndoto hii kubwa nadhani atakuwa amekwenda kufanya kazi nyingine kwa kuwa hatukujua wote kitakachofuata ni nini. Naomba niwashukuru wanangu wanne, Janeth, Fortunata, Herdwick na Namcy. Nawashukuru kwa sababu ni sehemu yangu, kwa sababu wanajua baba kapewa jukumu kubwa, naamini watanisaidia katika maisha ya kila siku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niwashukuru sana Wabunge kutoka Mkoa wa Rukwa. Nawashukuru kipekee kwa sababu nimekuwa nao, tumesaidiana mambo mengi na naamini hawatanitupa mkono hata katika hatua hii nzito. Nawashukuru sana wananchi wa Jimbo langu la Mpanda Mashariki na pia wananchi wote wa Mpanda kwa ujumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama cha Mapinduzi nawashukuru sana wana Rukwa wote. Ni imani yangu wataendelea kuniunga mkono, watanisaidia ili niweze kwa upande mmoja kumtumikia Rais vizuri lakini kwa upande mwingine niweze kutimiza wajibu wangu ndani ya Bunge hili kama mnavyotarajia. Nawaombeni sana Wabunge wenzangu tushikamane, tuheshimiane. Nina hakika tukienda kwa mtazamo huu Bunge hili lina uwezo kabisa wa kutimiza matarajio ya Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kushukuru viongozi wote wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maana ya viongozi wa Tanzania Bara na Tanzania Visiwani. Viongozi wote wa pande zote mbili wa Chama chetu cha Mapinduzi kwa kuwa na mimi. Sasa nitakuwa ni sehemu ya uongozi naamini watanisaidia kuniongoza vizuri na hivyo kuniwezesha kutimiza majukumu yangu inavyotakiwa.

Mheshim iwa Spika, nawashukuru sana Viongozi wa upande wa Vyama vya Upinzani na Wabunge wote kwa upande huo na kuwaomba tu kwamba kazi mliyonipa si nyepesi, kubwa na nzito lakini kwa namna nilivyoona nadhani tunaweza kufanya kazi iwe nyepesi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wote mliopiga kura kumsaidia Rais kunithibitisha nasema ahsanteni sana. Lakini nasema kwa dhati kabisa hata wale waliosema hapana, wajibu wangu ni kusema ahsanteni. Ninachoomba tu kwa wote waliosema ndiyo na waliosema hapana, tujue tu kwamba sisi wote ni Wabunge ndani ya Bunge hili na kwa hiyo tusaidiane kutimiza yale yote tunayotakiwa tuyatimize. Narudia kuwashukuruni sana (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, narudia kusema mimi si mwanasiasa wa siku nyingi kidogo na naamini nitaendelea kujifunza kutoka kwenu naamini vilevile kwamba katika mchakato huu wa kusimamia shughuli za wananchi tutaweza kabisa kwa pamoja kuleta kile ambacho Rais anasema maisha bora kwa kila Mtanzania. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, namalizia kwa kusema, inawezekana kabisa pakawa na hisia mbalimbali kutokana na taarifa ya Kamati yako Teule watu tukafikiri pengine kuna visa, ugomvi na nini lakini mimi nataka niamini kwamba kazi iliyofanywa kwa nia nzuri.

Niwapongeze na niwashukuru sana Mawaziri wenzangu waliokuwa katika jahazi hilo ambao wameungana na Mheshimiwa Waziri Mkuu kuomba wajiuzulu na mimi nasema hawa ni viongozi walioonyesha mfano kwa vitendo na sisi wengine yakitusibu ya namna hiyo namna peke yake ya kubadilika ni hiyo. Nawashukuru na nawasifu sana kwa uamuzi wao wa kijasiri waliochukua kukijenga Chama chetu cha Mapinduzi, lakini kujenga pia Taifa letu.

Mimi ni binadamu, nina mapungufu yangu, nitakuwa na kasoro zangu, kikubwa tuisite kuambiana, hakuna binadamu hata mmoja aliyekamilika. Nitashukuru sana kama katika utendaji wangu wa kazi nitawapata Ndugu zangu mniambie Mheshimiwa Waziri Mkuu hili sio sahihi, hili tunakuomba uache, hili mbona unakosea na mimi kwa utu uzima wangu nina hakika kabisa nitasema nimekusikilizeni na hili naacha. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, naomba basi wote tutoke na kauli moja. Baada ya kupokelewa kwa taarifa ile na kujadiliwa wote tuzamie tuseme yaliyopita si ndwele, sasa tugange yajayo. Nawashukuru sana na naomba Mwenyezi Mungu awabariki. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana. (*Makofî*)

SPIKA: Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge. Nawashukuru sana kwa kazi ya kumthibitisha Mheshimiwa Waziri Mkuu Mteule. Tumeifanya kwa ufanisi, sasa matangazo.

Semina ya kesho imefutwa, semina ya APR ile ya *African Pie Review Mechanism* imebidi tuifute. Aah, tuseme tumeahirisha, watakuwa tayari siku nyingine.

Jambo la pili, tunawatangazia pia Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri Mkoo wetu ataapishwa Ikulu Chamwino kesho tarehe 9 Februari, 2008 saa tano asubuhi.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tunakaribishwa na tuwe tumeketi katika viti vyetu pale Chamwino saa nne na nusu, kuna sehemu maalum imeandaliwa kwa ajili ya Waheshimiwa Wabunge. (*Makofi*)

Katibu ameandaa usafiri wa *minibuses* kwa baadhi ya wale ambao pengine watakuwa hawana usafiri wao, lakini kwa wale wanaojitegema wawayi, wakumbuke msururu unaweza kuwa mrefu pale langoni Chamwino.

Kwa hiyo, ukiambiwa kuketi saa nne na nusu asubuhi, sio maana yake saa nne na dakika ishirini na tano asubuhi, ndiyo bado uko kwenye lango la kuingilia, utakuwa umechelewa.

Kwa hiyo, kesho saa tano Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, anamwapisha Waziri Mkoo wetu Mteule, Mheshimiwa Mzenogo Kayanza Peter Pinda.

Taarifa kutoka vyanzo vya uhakika kabisa zimeniambia kwamba, Baraza la Mawaziri litatangazwa Jumatatu ijayo tarehe 11 Februari, 2008 na kuapishwa Chamwino tarehe 13 Februari, 2008, kwa maana hiyo Bunge haliwezi kukutana kwa kipindi hiki kwa sababu zile zile nilizokwishazieleza mapema na kwa sababu hizo basi, naomba sasa nilahirishe Bunge. Kabla sijafanya hivyo Kamati ya Uongozi naomba tukutane kesho mara baada ya kutoka Chamwino.

Waheshimiwa Wabunge, niseme wazi kwa sababu mimi ni muwazi, hali ilivyo ni kwamba tutabakiwa na siku mbili tu za kufanya kazi za Mkutano wa Kumi.

Siku mbili hazitoshii, sasa inabidi Kamati ya Uongozi tushauriane kwa sababu inawezekana baadhi ya ile Miswada ambayo bado haijapitishwa na Bunge, pengine inahitajika na tarehe ambayo inatakiwa Miswada hiyo iwe imepitishwa, mimi sijui. Hiyo itakuwa ni Serikali kutuambia. Kwa hiyo, Kamati ya Uongozi kesho saa nane.

Waheshimiwa Wabunge, nisisahau pia nimepata karatasi hapa ya Mbunge mmoja anasema:

Je, kutakuwa na sherehe ya kumpongeza Waziri Mkoo mpya na ni lini? Sasa mimi ninavyofahamu kwa kawaida ya Waheshimiwa Mawaziri Wakuu hawa sherehe zao wanazigharamia wao wenyewe.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkoo kama itakupendeza, basi kazi kwako sasa. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo, naliahirisha Bunge sasa hadi siku ya Alhamisi tarehe 14 Februari, 2008 hapa hapa Dodoma.

*(Saa 1.03 Usiku Bunge lilahirishwa Mpaka siku ya Alhamisi,
Tarehe 13 Februari, 2008 Saa Tatu Asubuhi)*